JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

MKOA WA SHINYANGA

Simu namba: 0784 278021
0783 359657
0757 765200

Shule ya Sekondari Shinyanga,
S.L.P. 157,

Mwadui Mines.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumbukumbu Namba: MKS/SHY/474/

**Tarehe 04/04/2022**

………………………………………………………………………

………………………………………………………………………

………………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023**

Ninafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule hii katika Kidato cha Tano 2022/23 na unatakiwa kufika tarehe………………… shuleni bila kuchelewa. Endapo hutafika ndani ya wiki mbili baada ya shule kufunguliwa bila kutoa taarifa nafasi yako atapewa mwanafunzi mwingine.

Shule ipo umbali wa kilometa 27 kutoka mjini Shinyanga uelekeo wa barabara iendayo Mwanza kupitia Maganzo. Ukija kwa gari moshi shuka Mjini Shinyanga upande basi/magari madogo yaendayo Maganzo/Mwadui, shuka Maganzo. Ukija kwa basi shuka kituo cha Maganzo, shule ipo upande wa Mashariki mwendo wa dakika 40 kwa kutembea kwa miguu. Kwa usafiri mwingine unaweza kutumia barabara inayoonyeshwa na kibao cha shule baada tu ya kupita shule ya Msingi Wame.

## MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE

1. **SARE ZA SHULE**

### (a) SARE YA DARASANI

1. Suruali mbili nyeusi (zenye marinda mawili kila upande) zisiwe za kubana/modo kwa chini upana suruali usipungue inchi 17-18.
2. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
3. Sweta ya bluu. Isiwe light blue au dark blue.
4. T-shirt ya bluu yenye kora.

5. Viatu vya ngozi nyeusi vya kufunga na kamba vyenye soli na visigino vifupi,Soksi jozi mbili (rangi ya nyeupe, nyeusi au khaki).

**(b) SARE YA KAZI ZA NJE**

i) Baada ya masomo (wakati wa kazi za nje na kushindia) sare inayovaliwa ni suruali nyeusi na T-Shirt ya bluu isiyo na kora.
ii) Track-suit ya rangi ya bluu yenye michirizi/misitari myeupe pemeni ya miguu na mikokononi na isiwe na nembo yeyote ya club ya mpira ila yaweza kuwa na nembo ya kampuni iliyoitengeneza.
iii) Uje na viatu vya wazi(open shoes) rangi nyeusi kwa ajili ya matumizi baada ya muda wa darasani.

**NB:** (i) T-shirt na tai zinapatikana kwenye maduka yaliyokaribu na shule , T-shirt, ya kola 15,000/= T-shirt isiyo na kora 10,000/=na tai 4,000/= kwa kila moja. (vinapatikana katika maduka yaliyo karibu na shule).

(ii) Usije na nguo za nyumbani wala **simu au laini ya simu** kwani ni kosa la kufukuzwa shule ukimiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi.

**(c) SARE YA MICHEZO**

Shule inasisitiza michezo kwa afya na makuzi bora.Hivyo uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili hiyo:-

1. Bukta mbili rangi ya bluu
2. Viatu vya raba vya kuchezea

**NB:**T-shirt isiyo na kora itatumika pia kwenye michezo.

2. **MALAZI**

Shule inatoa kitanda tu kwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga moja kwa moja. Kwa hiyo uje na:-

(i) Godoro dogo la “Sponge” lenye ukubwa wa 6’ x 2½‘ x 4’
(ii) Shuka mbili rangi ya Pink iliyokolea,mto na foronya mbili za Pink.
(iii) Kanda mbili jozi moja kwa ajili ya kuogea
(iv) Uje na mswaki, dawa ya mswaki, sabuni za kufulia na kuogea za kutosha muhula mzima
(v) Uje na chandarua kwa ajili ya mbu(light blue).
(vi) Uje na toilet paper zisizopungua 10 kwa matumizi yako(.

3. **VIFAA VYA KULIA CHAKULA**

Shule haina vyombo vya kulia, hivyo uje na sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya kuchukulia chakula na kulia, chakula chote kitaliwa katika bwalo la shule.

4. **FEDHA - (ADA NA MICHANGO)**

Malipo yafuatayo yafanyike katika Akaunti **Na.30701100013 NMB Jina la akaunti - Shinyanga Sekondari**. Mwanafunzi hatapokelewa shuleni akifika bila kuwa na Bank Pay-In-Slip ya malipo hayo, ambayo ni:-

(i) Karo ya shule Sh.35,000/= kwa Muhula au Sh.70,000 kwa mwaka
(ii) Sh.8, 000/= kwa ajili ya picha za "Passport Size" kwa ajili ya kitambulisho, matumizi ya ofisi na nembo ya shule.
(iii) Sh.10,000/= kwa ajili ya tahadhari ya mali ya shule ambayo hairudishwi (iv) Sh.35, 000/= kwa ajili ya mazingira na ukarabati wa Samani.
(v) Sh.25, 000/= kwa ajili Taaluma.
(vi) Sh.40,000/= kwa ajili ya vibarua wa shule(mhudumu wa ofisi, walinzi,wapishi,madereva na wazibua maji taka).
(vii) Uje na Ream Moja(01) ya karatasi (double A) A4 original
(viii) Uje na fedha kwa ajili ya matumizi yako binafsi, kama kununua vifaa vya kujisomea, usafi nakadhalika.
(ix) Kwa tahasusi za PCB,PCM na PGM uje na Reki, fagio la ndani,mopa na ndoo moja pia kwa tahasusi za HGL,HGE na EGM uje na kwanja, fagio la nje,Jembe na ndoo moja(01).

**N.B:** Malipo yanaweza kufanyika kwenye Tawi lolote la **NMB.**

5. Kabla ya kuingia shule hii utalazimika kupimwa na daktari aliyeajiriwa na Serikali. Fomu hiyo imeambatanishwa. Uje nayo shuleni ikiwa imekamilika
6. Uje na **Bima ya afya** kwa ajili ya matibabu.(ni muhimu sana)

7. Uje na nakala ya cheti cha matokeo ya kidato cha nne (result slip).

8. **URAIA:** Unatakiwa kuthibitisha kuwa wewe ni raia wa Tanzania au mkimbizi anayetambulika na Serikali ya Tanzania. Njoo na uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Wilaya yako au cheti chako cha kuzaliwa.

9. **SHERIA ZA SHULE:** Baadhi ya sheria za shule zimeambatanishwa na barua hii. Itabidi uzisome na kuzielewa ili uzifuate kikamilifu la sivyo hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako. Kwa ujumla heshima (nidhamu) juhudi ya kazi na maarifa katika maisha ya shule ni msingi wa mafanikio. ***Moto wa shule* – "ELIMU NI MSINGI WA MAFANIKIO BORA"**.

10. Fomu ya kukubali kuandikishwa na ahadi ya utii imeambatanishwa. Ijazwe na kuletwa shuleni kwa Mwalimu Mwandamizi Malezi na Utamaduni.

**N.B** Unashauriwa kununua vitabu vilivyopendekezwa kwenye orodha iliyoambatanishwa kulingana na tahasusi yako.

Nakukaribisha sana katika shule ya Shinyanga Sekondari yenye mazingira mazuri ya kitaaluma.

..........................

Bernard I.Leonard
Mkuu wa Shule

HEADMASTER
SHINYANGA TECHNICAL SCHOOL

# SHERIA ZA SHULE

1. Mwanafunzi awe na bidii ya kujielimisha na kufanya mazoezi na majaribio yote darasani na mitihani yote ikiwemo ya nje

2. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa. Makazi na nyumba za wafanyakazi na Kanisani (Mt. Paulo Parokia ya Shy-bush) na msikitini (wakati usio wa sala) ni nje ya mipaka ya shule.

3. Shule ina sare za aina mbili; ya darasani na ya kazi za nje. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa nguo za nyumbani, pia ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule amevaa sare ya kazi za nje. Sare ya viatu ni ngozi nyeusi ya kufunika. Viatu vya wazi, makoti na majaketi ni marufuku.

4. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wakubwa na wadogo ndani na nje ya shule. Atasimama na kuwasalimu kwa heshima wanapopita au kuingia katika chumba alimo.

5. Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi wa mwili, nguo, mazingira na lugha. Pia ni marufuku kuvaa kofia, kunyoa upara na kufuga ndevu.

6. Wageni wa jinsia zote hawaruhusiwi kukaribia, kuingia au kulala mabwenini.

7. Ni lazima mwanafunzi afuate ratiba kama itakavyotolewa na viongozi wa shule

8. Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni siku ya kufungua, au siku moja kabla ya kufungua shule. Kuchelewa kufika shuleni ni uvunjaji wa sheria ya Elimu Na.25 ya 1978 sehemu 60(0) aya ya 6(1) na sheria za shule.

9. Mwanafunzi anatakiwa kutunza vema mali ya umma na yake binafsi.

10. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoa habari zozote zinazohusu shule kwa vyombo vya habari au watu wasiohusika bila ruhusa ya Mkuu wa shule. Mwanafunzi akivunja sheria hii ni kosa la kufukuzwa shule mara moja.

11. Chakula chote kitaliwa ndani ya bwalo la chakula. Kuvunja sheria hii kutasababisha mwanafunzi kuchukuliwa hatua kali ikiwemo kusimamishwa masomo.

12. Nimarufuku mwanafunzi kuwa na simu au kumiliki laini ya simu. Kuvunja sheria hii kutasababisha mwanafunzi kuchukuliwa hatua kali ikiwemo kusimamishwa masomo

13. Tahadhari: Mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule mara moja akipatikana na makosa yafuatayo:-

    Wizi, uasherati na ushoga, ubakaji, ulevi wa pombe, madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, sigara, cocaine, mirungi, kubeli n.k. kupigana au kupiga, kuharibu kwa makusudi/uzembe mali ya umma/shule, kuwa nje ya shule baada ya saa 12.00 jioni na kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule, kudharau Bendera ya taifa, kuoa, kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu, kukataa adhabu kwa makusudi.

    NB: Kila mwanafunzi anatakiwa awepo wakati wa "kuitwa majina" (Roll call) saa 12.00 jioni kwa siku za Jumamosi, Jumapili na siku za siku kuu. Au wakati wowote atakapohitajika.

14. Mwanafunzi anatakiwa afuate sheria za nchi ya Tanzania na viongozi wake/mamlaka mbalimbali. Huu ni wajibu wa raia/mzalendo

## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwaujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtuyeyote yule.

(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote na siyokunyoa kipara.

(vii) Kufuga ndevu.

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

(ix) Uvutaji wa sigara.

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa

(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunjasheria za nchi.

(xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana

(xiii) Kutembelea majumba ya starehe na vyumba za kulala wageni

(xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira yashule.

(xv) Kudharau Bendera ya Taifa

(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNLOJIA

SHULE YA SEKONDARI SHINYANGA FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE (Ijazwe kwa herufi kubwa na irudishwe kwa mkuu wa shule)

*Picha ya Mzazi/Mlezi*

*Picha ya Mwanafunzi*

1. Jina kamili…………………………………………………………………………………………………..
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………..Wilaya……………………………….
3. Taifa……………………………………………………………………………………………………..Shule unayotoka…………………………………………………………………………………..........

AHADI ZA MWANAFUNZI

(a) Naahidi kutii na kuzifuata sheria zote za shule kama zilivyoambatanishwa.

(b) Naahidi kuwa sitathubutu kuanzisha wala kushiriki katika mgomo wa aina yoyote ile hapa shuleni.

(c) Naahidi kuwa nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa mbele ya uongozi wa shule endapo nitasikia tetesi au taarifa ya kuaminika juu ya jambo lolote linaloashiria kuleta vurugu au ukosefu wa amani shuleni. Pia nitafuata utaratibu wa kumaliza matatizo shuleni kwa kutumia vikao halali.

(d) Naahidi kutotoka nje ya eneo la shule kwa kipindi chote cha kuwepo kwangu hapa shuleni na kutokukaribisha mgeni yeyote kukaa ama kulala bwenini bila idhini ya uongozi wa shule.

(e) Naahidi kuwa sitavaa suruali za kubana (Vimodo), kofia pamoja na nguo ambazo si sare ya shule (nguo za nyumbani).

(f) Vile vile naahidi nitakula chakula kilichoandaliwa siku husika kutokana na utarabitu wa shule.

(g) Naahidi na kuamini kwamba dhumuni langu kuwa hapa shuleni ni kupata elimu na si vinginevyo.

(h) Naahidi nitafanya mazoezi yote, majaribio yote, mitihani yote ya nje na ndani (Mock and National Examination).

(i) Ninaahidi kuwa nitashiriki bila kukosa masomo ya usiku (Night Preparation) kufuatana na ratiba ya shule darasani kwangu.

Mimi ……………………………………………………………. Kidato cha …………………………….

Baada ya kusoma kwa makini na kuelewa sheria za shule na ahadi za mwanafunzi zilizowekwa na Uongozi wa shule. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu pamoja na Mkuu wa Shule kuwa nitazitii; kuzingatia; kutekeleza na kufuata sheria zote za shule na kwamba nikizivunja sheria za shule nijihesabu nimejifuta shule mwenyewe.

Jina kamili na sahihi ya mwanafunzi ………………………………………… Tarehe ………………….

Jina kamili na sahihi ya Mzazi/mlezi wangu……………………………… Tarehe ………………….

Namba ya simu ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………………..

Taja jina la mtu wa karibu ambaye shule inaweza kuwasiliana nae kwa jambo lolote iwapo

mzazi/mlezi akikosekana
Jina kamili………………………………………………………………..Anwani…………………………………..……………….
namba yake ya simu……………………………………………….

Jina/sahihi ya Mkuu wa Shule …………………………………………………Tarehe…………………………..

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY STUDENT MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government Medical Officer and returned to the Headmaster, Shinyanga Secondary School)

……………………………………………………………………………………………………

Please examine the student named above and comment on his/her health by responding to the following items. Kindly put a tick in front of each item either YES or NO.

1. Does the student have problems in connection with:-

   A. Sight? …………………………………………………………………… 1. NO
      If YES state: ……………………………………………………………… 2. YES

   B. Hearing? ………………………………………………………………… 1. NO If YES
      state: …………………………………………………………… 2. YES

   C. Speech? ………………………………………………………………… 1. NO If YES
      state: …………………………………………………………… 2. YES

   D. T.B? …………………………………………………………………… 1. NO
      If YES state: ……………………………………………………………… 2. YES

   E. Blood Pressure? ……………………………………………………… 1. NO
      If YES state: ……………………………………………………………… 2. YES

   F. Any Physical disability? ………………………………………………… 1. NO If YES
      state: …………………………………………………………… 2. YES

   G. Any other health problem? …………………………………………… 1. NO
      If YES state: ……………………………………………………………… 2. YES

2. Do you therefore recommend the said student medically fit for studentship at this school

   If NO. Please state ……………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………………………

……………………………………………… ……………………………………………

NAME AND SIGNATURE DESIGNATION

……………………………………………… ……………………………………………

DATE STAMP

***THIS FORM TO BE FILLED WITH LEARNES WITH SPECIAL NEEDS ONLY***

### *1. PERSONAL PARTICULARS*

PASSPORT

NAME: Surname: ……………………………………..

First name: ………………………………….. Middle name: ……………………………….

Date of birth: Date: ….. Month: …….Year: …………… Sex…………..

Citizenship: …………………………….

Language: ………………………………

Tribe: …………………………………..

Religion: ……………………………….

Type of disability: ……………………..

### *2. CONTACT ADDRESSES*

Home address: ………………………………

Current address: ……………………………

Mobile number: …………………………….

Email address: ………………………………

### *3. REFFEREES & CARE GIVERS*

Name of parent or institution: ……………………………………………………….

Address: ………………………………

Email: …………………………………

Phone number: ………………………..

### *4. CERTIFICATION*

I, **……………………………………………..**certify that to the best of my knowledge the information given are correct.

……………………. ……………………

**E.KALIMANZIRA**
**HEAD OF SPECIAL. ED. DEPARTMENT**

**B.I.LEONARD**
**HEADMASTER**

## ORODHA YA VITABU

| NA | IDARA | VITABU |
|---|---|---|
| 1. | HISTORY | 1. Advanced level history paper one & two by Zisti Kamili.<br>2. Understanding African history. Advanced level paper one by Joannes Biginuamungu & George Tumani.<br>3. Mastering advanced level history book One & Two (2010) by Kato, A.<br>4. Contemporary history events. paper 1 &2 BY Shibitali C.K<br>5. History from 5&6 by Scsu & MoEVT-Zanzibar |
| 2. | GEOGRAPHY | 1. A practical Guide to statistical Maps and Digrams by H.C.Truman<br>2. Practical geography for Africa by J.M.Pritchard<br>3. Principle of physical geography by F.J.Monkhouse 4. Human and economic geography by D.T. Msabila<br>5. Map reading by Zisti Kamili.<br>6. Photo interpretation by Kura<br>7. Physical geography A-Level by D.T Msabila<br>8. Physical geography by R.Bunnet<br>9. Introducing physical geography and map reading by Simon Ross |
| 3. | ENGLISH LANGUAGE | 1. Advanced literature by Nyambari Nyangwine<br>2. The real English Advanced level by Dr. Michael Kadeghe.<br>3. New advanced level English by Charles E. Shalua<br>4. Introduction of phonology by Gimson<br>5. A University grammar of English<br>6. A complete English course for form V & VI by Dr. Michael Kadeghe<br>7. Oxford advanced learners dictionary |
| 4. | ECONOMICS | 1. Modern Economic by Dr. Dewit<br>2. Modern economic by Robert pandic<br>3. Principle of economic by Jinghan<br>4. Simplified Economic by saalem |
| 5. | MATHEMATICS | 1. Advanced mathematics by L.K Turner I&II.<br>2. Advanced mathematics by C.J. Tranter.<br>3. Advanced mathematics by L.K. Shayo<br>4. Advanced mathematics by Backhouse Vol. I & II 5. Advanced mathematics Vol I &II by S.Chand.<br>6. Understanding pure mathematics by A.J. Sadler & D.W.S. Thorning<br>7. Electronic calculators (Scientific Function 991) |
| 6. | PHYSICS | 1. Advanced level physics by M.Nelkon & P.Parker<br>2. Concise “A” Level physics by Arwahyser.<br>3. Physics by Tom Duncan<br>4. New intermediate physics<br>5. Rodger Muncuster by Rodger Muncuster<br>6. Calculation of Advanced level physics by Tllower and J.F. Rounce |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | CHEMISTRY | 1. A level chemistry by E.N.Ramsden<br>2. Advanced level inorganic chemistry Part I & II<br>3. Organic chemistry part A &B by Tanzania publishing House<br>4. Physical chemistry by Mzumbe<br>5. Advanced level chemistry by Ramsden |
| 8. | BIOLOGY | 1. Biology science by Taylor et al (cambridge)<br>2. Advanced biology by Sinpkins (ELBS)<br>3. Understanding Biology by Co Susan Trole<br>4. Understanding Biology by Nelson Thornes |
| 9. | KISWAHILI | 1. SAMIKISA (semina za kimataifa).<br>2. SAMAKISA(semina za kimataifa).<br>3. Nadharia ya Uhakiki.<br>4. Kiswahili kidato cha tano na sita(Lugha na Sarufi).TIE<br>5.Kiswahili kidato cha tano na sita(Fasihi).TIE |